*Mulika, Na. 42 (2), 184-196*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Utabirifu wa Makosa ya Utenganishaji na Uunganishaji wa Maneno katika Kiswahili

*Rehema Stephano*[1]
Chuo Kikuu cha Dodoma

**DOI**: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t2.3

**Ikisiri**

Uandishi ni mchakato unaohitaji umakini ili kinachoandikwa kieleweke kwa msomaji kwa namna iliyokusudiwa na mwandishi. Ikiwa kueleweka kutazingatiwa, basi, kutakuwa na mawasiliano madhubuti. Hata hivyo, matini mbalimbali zimekuwa na makosa mengi kiasi cha kukwamisha mawasiliano baina ya mwandishi na msomaji wake. Lengo la makala haya ni kuchunguza utabirifu wa makosa katika uandishi kwa kumakinikia makosa ya utenganishaji na uunganishaji wa maneno. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder (1967) imetumika kuchambua na kujadili data za utafiti kwa sababu inahusika na makosa yanayohusiana na lugha na isimu. Data zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini na usaili. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba makosa ya kutenganisha na kuunganisha maneno yanatabirika kwa sababu yana uelekeo mmoja. Makosa ya kuunganisha maneno yamegawanyika katika makundi makubwa manne, yaani maneno yenye urejeshi, maneno yenye kiambishi cha umahali na wakati, maneno yanayotokana na uradidi, na maneno ambatani. Makosa ya kuunganisha maneno yamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni mwambatano wa vitenzi shirikishi vya “kuwa na” na nomino, na viunganishi tegemezi vinavyoanza na “kwa”. Kwa ujumla, makosa haya yanatokana na uhamishaji wa kanuni moja katika uandishi wa maneno fulani yenye vipashio, hususani viambishi vinavyofanana. Kufuatia matokeo haya, makala haya yanapendekeza waandishi kuzingatia aina na sifa mahususi za maneno na si kujumuisha kanuni zinazotumika kuandika baadhi ya maneno.

## 1.0 Utangulizi

Uandishi ni stadi muhimu katika mawasiliano. Kwa hiyo, unahitajika umakini ili jambo linalowasilishwa kwa njia ya maandishi liweze kueleweka kwa mtu aliyekusudiwa kulisoma kwa namna ileile ambavyo mwandishi aliikusudia. Mara nyingi, matini zimekuwa na makosa mengi kiasi cha kukwamisha mawasiliano baina ya mwandishi na msomaji wake. Miongoni mwayo ni makosa ya kisintaksia, kitahajia, kiuteuzi wa maneno, kiuakifishaji, kuunganisha na kutenganisha maneno (Wangila, 2017; Mpemba, 2018; Stephano, 2019; Lupogo, 2020; Mushumbwa, 2022).

[1] Baruapepe: rest_tz@yahoo.com

Pamoja na aina mbalimbali za makosa kuchunguzwa na kujadiliwa, katika Kiswahili, makosa ya kutenganisha na kuunganisha maneno bado hayajachunguzwa vya kutosha. Makosa hayo yanatajwa kwamba ni miongoni mwa makosa makubwa ambayo yamezoeleka kufanywa na waandishi (Kohsom na Gobet, 1997; Mpemba, 2018; Lupogo, 2020; Mushumbwa, 2022). Baadhi ya wataalamu wameyajadili makosa haya kwa kuyahusisha na makosa ya tahajia (Wangila, 2017). Wengine wameyahusisha na unafasishaji baina ya neno na neno (Mpemba, 2018). Mpemba anaeleza kwamba tatizo kubwa la unafasishaji linalowakabili waandishi wa matini za Kiswahili ni la kuweka nafasi kati ya neno na neno, ambapo maneno mawili na kuendelea huunganishwa, na neno moja ambalo halitakiwi kutenganishwa hutenganishwa.

Makosa ya aina hii, kama ilivyo kwa aina zingine, yana madhara katika uandishi pia. Baadhi ya madhara hayo ni kusababisha msomaji, ama kushindwa kuelewa ujumbe uliomo katika andiko, au kumpa uzito na kupunguza kasi ya usomaji (Oralova na Kuperman, 2021). Kutokana na hali hiyo, humlazimu msomaji kuwa makini kutambua maneno yaliyounganishwa na kutenganishwa pamoja na maana zake; la sivyo, hawezi kuelewa kilichoandikwa.

Wataalamu wanaona kwamba makosa haya huchangiwa na sababu kadhaa kama vile mazoea, hasa yatokanayo na uandishi huria wa matini ambazo si rasmi (Wangila, 2017; Lupogo 2020). Uandishi huo huria, kwa hiyo, huhamishiwa kwa namna ileile katika uandishi rasmi. Sababu zingine ni waandishi kutojua kwamba kutounganisha/kuunganisha baadhi ya maneno ni makosa, kukosa umakini, kuambukizana kufanya makosa, yaani mtu akisoma kazi iliyoandikwa kwa makosa anajua ndivyo maneno yanavyotakiwa kuandikwa kumbe ni makosa, pamoja na ujumuishaji wa kanuni za lugha (Lupogo, 2020). Aidha, wataalamu wengine wanadai kuwa kosa la kutenganisha maneno husababishwa na waandishi kutatizwa na urefu wa neno hata kulazimika kutenganisha viambishi na mashina yake (Mushumbwa, 2022). Sababu hii ina mashaka kwa sababu maneno kama vile *wa ‘‘nne*” (wanne), na “*lililo leta*” (lililoleta) ambayo Mushumbwa anayatolea mfano ni mafupi kuliko neno “*wanashambulia’’*.

Ingawa tafiti zilizokwishafanyika zimeshughulikia makosa ya kutenganisha na kuunganisha maneno, bado hayakukundishwa na hazikutolewa sababu zenye mwelekeo tabirifu kuhusu kutendeka kwa makosa hayo. Watafiti waliotangulia hawakuonesha mazingira yenye mwelekeo mmoja yanayochangia makosa ya aina moja kutokea katika kazi za uandishi. Makala haya yameyaainisha, yameonesha jinsi yanavyotokea kwa namna ileile katika uandishi, sababu za kufanyika na kupendekeza namna ya kutatua makosa hayo kwa kuzingatia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.

## 2.0 Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder (1967) ambayo imeendelezwa na Gass na Selinker (2008) imetumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data za makala haya. Wafuasi wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa wanaitumia kuchambua makosa yanayohusiana na isimu kwa ujumla bila kujali ni ya wajifunzaji wa lugha ya pili au yanafanywa na waandishi wowote wale. Nadharia hii inapendekeza hatua sita za kuchambua makosa ya kiisimu. Hatua hizo ni kukusanya sampuli ya data zinazohusiana na makosa ya kiisimu, kutambua makosa, kubainisha kategoria za makosa, kuonesha msambao wa makosa, kufafanua sababu za makosa, na kupendekeza njia za kutatua makosa. Katika makala haya, hatua zote zinazopaswa kufuatwa katika kuchambua makosa zimetumika ikizingatiwa kwamba makosa ya kutenganisha na kuunganisha maneno ni ya kiisimu.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Data zilizotumika katika makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni uchambuzi wa matini na usaili. Insha 20 za wanafunzi wa uzamili wa Chuo Kikuu cha Dodoma zilichambuliwa ili kubaini makosa mbalimbali ya utenganishaji na uunganishaji wa maneno kwa lengo la kukidhi hatua ya kwanza ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Wahadhiri watano (5) wa masomo ya lugha na isimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma walisailiwa, lengo likiwa kutambua, kufafanua sababu na kupendekeza njia za makosa ya kutenganisha na kuunganisha maneno kulingana na matakwa ya nadharia teule pia. Usampulishaji lengwa ulitumika kuwapata wahadhiri hao kwa sababu utafiti ulilenga watafitiwa wenye ubobevu wa lugha na isimu, na si vinginevyo.

## 4.0 Makosa ya Uunganishaji na ya Utenganishaji wa Maneno

Utafiti umebaini kwamba, miongoni mwa makosa yanayofanywa na waandishi ni kuunganisha na kutenganisha maneno. Kila aina ya kosa ina aina zake za makosa, lakini aina hizo zina mwelekeo unaotabirika.

### 4.1 Utenganishaji wa Maneno

Utenganishaji wa maneno unaojadiliwa katika makala haya una mielekeo ya aina tatu. Mwelekeo wa kwanza ni wa maneno yenye urejeshi. Mwelekeo wa pili unahusu maneno yanayotokana na uradidi. Mwelekeo wa tatu ni wa maneno ambatani. Mielekeo yote inatabirika kwa sababu makosa ya aina zote yanatokea kwa namna inayofanana.

#### 4.1.1 Maneno yenye Urejeshi

Urejeshi ni hali ya mofu kumrejea mtenda, ambapo kunakuwa na viambishi, hasa katika vitenzi ambavyo vinawakilisha kitajwa, yaani nomino inayohusika na tendo (Kihore, Massamba na Msanjila, 2012). Kitenzi cha Kiswahili ni ambishibainishi, yaani kinaambikwa viambishi mbalimbali mwanzoni na mwishoni, ambapo kila

kiambishi kina dhima tofauti na kiambishi kingine. Kiambishi cha urejeshi ni mojawapo ya viambishi hivyo. Kwa mujibu wa wanaisimu wa Kibantu, kiambishi cha urejeshi kipo kati ya ruwaza ya tano (5) (Kiango, 2000), au ya sita (6) (Polomé, 1967) katika mpangilio thabiti wa viambishi vinavyoambatana na mzizi wa kitenzi. Pamoja na tofauti za nafasi ya ruwaza ya kiambishi hicho, bado wataalamu wote wanakubaliana kwamba ni kiambishi awali. Katika Kiswahili, mofu ya urejeshi huendana na ngeli ya nomino; mathalani, kama ni ngeli ya mu/m/mw - wa, kiambishi cha urejeshi kitakuwa -ye- kwa umoja, na -o- kwa wingi. Kwa vile ni kiambishi, mofu mojawapo katika viambajengo vya kitenzi, haipaswi kutenganishwa na mzizi wa kitenzi hicho. Hata hivyo, utafiti uliofanyika umebaini kwamba baadhi ya waandishi wanatenganisha shina la kitenzi na viambishi vinavyokitangulia kama inavyojibainisha katika Jedwali Na. 1:

**Jedwali Na. 1: Utenganishaji wa Maneno yenye Urejeshi**

| Na. | Neno Lililotenganishwa | Matini Lilimotokea |
|---|---|---|
| 1. | ulio pendekezwa (uliopendekezwa) | Mkutano **ulio pendekezwa** umeahirishwa. |
| 2. | vilivyo chaguliwa (vilivyochaguliwa) | Vikundi **vilivyo chaguliwa** vimeandikiwa barua. |
| 3. | vinavyo muwezesha (vinavyomwezesha) | Vitu **vinavyo muwezesha** mwanafunzi kujitegemea ni kujisomea kwa bidii. |
| 4. | yatakayo zingatiwa (yatakayozingatiwa) | Mambo **yatakayo zingatiwa** ni ujengaji wa hoja na ushikamani. |
| 5. | zinazo bainisha (zinazobainisha) | Sehemu **zinazo bainisha** aina mbalimbali za maneno ... |
| 6. | Alilo lima (alilolima) | Shamba **alilo lima** halina rutuba. |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2023)

Jedwali Na. 1 linaonesha maneno yakiwa yametenganishwa katika mpaka wa kiambishi cha urejeshi na shina la kitenzi. Kuna namna kuu tatu za kutumia kiambishi cha urejeshi. Aina ya kwanza ni kuweka kiambishi katika kijineno amba-. Mfano wa urejeshi wa aina hii ni “*amba**ye*** ameondoka arudi upesi”, na “kiatu *amba**cho*** kimepotea ni changu”. Aina ya pili ni kuweka kiambishi cha urejeshi kabla ya mzizi wa kitenzi kama ilivyo katika maneno “mwanafunzi *ali**ye**mchapa* mwenzake aadhibiwe”, na “mlango *uli**o**funguka ufungwe”*. Aina ya mwisho ni kuweka kiambishi cha urejeshi mwishoni mwa kitenzi kama ilivyo katika “*aisifu**ye*** mvua imemnyea”, na “shamba *wakodisha**lo*** limekosa rutuba”.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba makosa yanatokea katika maneno ambayo yanawekwa kiambishi cha urejeshi kabla ya mzizi kama ambavyo pia Mushumbwa (2022) amefafanua katika utafiti wake. Kwa mujibu wa usaili uliofanyika,

waandishi wanafanya kosa la kutenganisha maneno yenye urejeshi kwa sababu kubwa mbili. Mosi, wanashindwa kutofautisha urejeshi unaowekwa kabla ya mzizi wa kitenzi na ule unaowekwa mwishoni mwa kijineno *amba-*. Urejeshi unaotokea katika kijineno *amba-* hufuatiwa na kitenzi ambacho huwa na kiambishi cha hali au njeo, ilhali katika kitenzi kinachowekwa kiambishi cha urejeshi kabla ya mzizi, viambishi vyote vyenye dhima tofautitofauti huambatishwa kwenye kitenzi moja kwa moja, hivyo, kuunda neno moja na si maneno mawili tofauti.

Pili, utafiti umebaini kuwa waandishi wanashindwa kutofautisha viambishi na viwakilishi (vyenye kiambishi cha urejeshi) katika mwandamano wa vitenzi na nomino. Kiwakilishi (chenye kiambishi cha urejeshi) huweza kusimama peke yake kikifuatiwa na maneno mengine kama ilivyo katika "*asi**ye** mrefu* hawezi kuangua" au "*asi**ye** mwalimu* asifundishe". Kiwakilishi rejeshi hurejesha tendo kwa mtenda au kwa mtendwa. Viwakilishi vya aina hii vimegawanyika katika makundi mawili, vile vinavyoundwa kwa mzizi *amba-* na vile vinavyoundwa na kiambishi cha urejeshi kulingana na ngeli husika (Mohamed, 1998; Khamis, 2009; Kihore, 2009).

Lupogo (2020) anafafanua kwamba waandishi hujumuisha kanuni kwa vile viambishi wanapokatishia neno huweza kuwa neno linalojitegemea katika baadhi ya miktadha kama ilivyo katika "*asi**ye*** na mke hana furaha", "*pali**po*** na wengi hapaharibiki jambo" na "*wali**mo*** wazee ni pazuri". Ingawa Lupogo hafafanui miktadha hiyo, utafiti uliofanyika umebaini kwamba hivyo ambavyo anaviita viambishi vinavyoweza kusimama kama maneno si viambishi, bali ni maneno aina ya viwakilishi. Kwa upande mwingine, makala haya yanaonesha kwamba viambishi vinavyoongozana na kiambishi cha urejeshi haviwezi kusimama peke yake ikiwa vinafuatiwa na mzizi wa kitenzi. Kwa maneno mengine, hivyo ni viambishi, si maneno (viwakilishi). Mushumbwa (2022) anadai kwamba viambishi haviwezi kusimama peke yake, bali huunganishwa na mashina ya maneno ndipo vipate uamilifu. Kwa hiyo, kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, waandishi wanapaswa kutofautisha viambishi na maneno katika uandishi ili kuepuka kutenganisha maneno na viambishi vyake, hasa vitenzi vyenye viambishi vya urejeshi kabla ya mzizi.

#### 4.1.2 Maneno yenye Kiambishi cha Umahali na Wakati

Katika Kiswahili, kama ilivyo kwa lugha zingine za Kibantu, kuna viambishi vya umahali vitatu ambavyo ni *-po-*, *-mo-*, na *-ko-*. Viambishi hivi vinatokana na ngeli ya mahali *pa-*, *ku-*, *mu-* (Kihore, Massamba na Msanjila, 2012). Kiambishi *-po-* huhusu mahali mahususi, *-ko-* huhusu mahali pa jumla na *-mo-* huhusu mahali ndani ya kitu fulani (Mohamed, 1998). Kiambishi *-po-* pia huweza kuwakilisha wakati katika tungo. Viambishi hivi vya umahali na vya wakati huweza kuambatishwa na mzizi wa neno kwa vile Kiswahili ni lugha ambishibainishi. Makala haya yanaonesha kuwa waandishi hutenganisha mzizi wa kitenzi na viambishi vingine vinavyoambatana na viambishi vya umahali na wakati. Jedwali Na. 2 linathibitisha hoja hii:

**Jedwali Na. 2: Utenganishaji wa Maneno yenye Viambishi vya Umahali na Wakati**

| **Na.** | **Neno Lililotenganishwa** | **Matini Lilimotokea** |
|---|---|---|
| 1. | Alipo anguka (alipoanguka) | **Alipo anguka** wanafunzi wenzake walimkimbilia na kumnyanyua. |
| 2. | Wanapo kaa (wanapokaa) ni mbali | Baba na mama **wana pokaa** ni mbali. |
| 3. | Alipo kaa (alipokaa) | **Alipo kaa** pana vumbi sana. |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2023)

Mifano iliyomo katika Jedwali Na. 2 inaonesha jinsi maneno yenye viambishi vya umahali na vya wakati yanavyotenganishwa pale kwenye viambishi tajwa na sehemu nyingine inayofuata ya neno ambayo ni mzizi. Makala haya yanaonesha kuwa kosa hili linafanana na lile la utenganishaji wa viambishi vinavyoambatana na vitenzi katika kiambishi cha urejeshi na mzizi wa kitenzi. Utafiti umebaini kwamba viambishi vya umahali, kutokana na kuwa na sauti -*o*- vinafananishwa na viambishi vya o-rejeshi, ndio maana vinatenganishwa kwa namna ileile kama ilivyo kwa vitenzi vyenye viambishi vya urejeshi. Viambishi vya umahali na vya wakati huweza kuambikwa kwa namna tatu kama za kiambishi cha o-rejeshi, yaani kuambikwa kwenye kijineno *amba*- (mfano *amba**po***, *amba**ko***, na *amba**mo***), kuweka kabla ya mzizi wa kitenzi (*ali**po**lala*, *ali**mo**kaa*, *ana**ko**kaa* na *ali**po**ondoka*) na kuwekwa mwishoni mwa kitenzi (*alala**po***, *akaa**mo***, *akaa**po***, *akaa**ko*** na *aondoka**po***). Kutokana na kufanana kwa uambikaji wa viambishi vya urejeshi na vya mahali na wakati, ni dhahiri kuwa jambo hili ni lazima litokee kwa viambishi vya aina zote kwa namna moja. Makala haya yanapendekeza kwamba, viambishi hivi vinapotokea kabla ya mzizi wa kitenzi, ni lazima viungane na mzizi wake kwa sababu, vikisimama peke yake, haviwezi kuleta maana. Maana ya viambishi hivyo inapatikana vinapoambatishwa na mizizi yake (Mushumbwa, 2022).

### 4.1.3 Maneno Yanayotokana na Uradidi

Uradidi ni mojawapo ya mbinu zinazotumika kuunda maneno. Neno au sehemu ya neno hurudiwa kwa lengo la kuunda neno lingine (Rubanza, 1996). Kwa hiyo, kuna aina mbili za uradidi, yaani uradidi kamili na uradidi nusu. Uradidi kamili unahusu kurudia neno zima kama lilivyo kwa lengo la kuunda neno lingine. Uradidi nusu unahusu kurudia kipande cha neno na kukiunganisha na neno lake kamili ili kuunda neno lingine. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa maneno yanayotokana na uradidi yanatenganishwa katika uandishi, ambapo aina zote za uradidi zinakumbwa na kosa la kutenganisha maneno. Mifano iliyomo katika Jedwali Na. 3 inaonesha makosa hayo:

**Jedwali Na. 3: Utenganishaji wa Maneno Radidi**

| Na. | Neno Lililotenganishwa | Matini Lilimotokea |
|---|---|---|
| 1. | Tofauti tofauti (tofautitofauti) | Kuhitilafiana huko kumepelekea kuibuka kwa mitazamo **tofauti tofauti** … Kwa ujumla, lahaja ni namna **tofauti tofauti** za kuizumgumzia lugha moja. |
| 2. | Kubadilika badilika (kubadilikabadilika) | Msamiati huo ni majina ya hali za kimaumbile au vitu ambavyo ni vya kawaida katika maisha ya kila siku na ambavyo havina kawaida ya **kubadilika badilika**. |
| 3. | Mbali mbali (mbalimbali) | Mbinu ambazo zimetumika katika ukusanyaji wa data ni pamoja na ile ya uchunguzi matini ambapo machapisho **mbali mbali** … |
| 4. | Wameandika andika (wameandikaandika) | Wataalamu mbalimbali **wameandika andika** kuhusu ruwaza za kitenzi cha Kiswahili. |
| 5. | Kujirudia rudia (kujirudiarudia) | **Kujirudia rudia** kwa tatizo hili linafanya nichunguze sababu zinazosababisha mitazamo kuhusu ruwaza za Kibantu kutofautiana. |
| 6. | Ndogo ndogo (ndogondogo) | Jamii **ndogo ndogo** za lugha humezwa na jamii lugha kubwa. |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2023)

Jedwali Na. 3 linaonesha namna maneno yanayotokana na uradidi yanavyotenganishwa kimakosa na waandishi. Kulingana na mbinu ya uundaji wa maneno ya urudufu, neno moja linaundwa kutokana na kurudiwa kwa neno kamili au kurudiwa kwa sehemu ya neno hilo, na kinachopatikana ni neno (moja) na sio maneno mawili. Kwa sababu linaloundwa ni neno moja, na si maneno kadhaa, linapaswa kuandikwa bila kutenganishwa. Kamwe isichukuliwe kuwa ni maneno mawili. Hii ni kwa sababu neno linaloundwa, aghalabu, huwa na maana tofauti na ya neno la awali lililorudiwa (Kiango, 1995). Kwa mfano, neno **mbali** maana yake ni masafa marefu baina ya mahali na mahali, hatua au mwendo mrefu, lakini neno **mbalimbali**, ambalo limetokana na kukaririwa kwa neno **mbali**, maana yake ni isiyofanana, isiyohusiana, tofauti au pasipo kukaribiana au kuchanganyika (TUKI, 2019). Vilevile, maana ya neno la awali linalokaririwa inaweza kurekebishwa kwa kuimarishwa au kudhoofishwa kama anavyosema Mnenuka (2010). Kwa hiyo, kwa mujibu wa makala haya, kwa kuyatenganisha maneno yaliyoundwa kwa njia ya uradidi, msomaji anaweza kupata maana inayotokana na neno mojamoja au asielewe kabisa kulingana na muktadha wa tungo.

### 4.1.4 Maneno Yanayotokana na Uambatanishaji

Uambatanishaji ni kitendo cha kuunganisha maneno mawili au zaidi kwa lengo la kuunda neno moja. Neno hili huwa na maana tofauti na maana zinazotokana na maneno yaliyotumika kuliunda neno hilo (TET, 2019). Mfano ni mwana + harakati (mwanaharakati), bata + mzinga (batamzinga), pilipili + kichaa (pilipilikichaa) na kitinda + mimba (kitindamimba). Kuna aina kuu mbili za maneno ambatani ambazo ni maneno ambatani sahili na maneno ambatani changamani (Booij, 2007; Lieber, 2009; Ralli, 2013). Maneno ambatani sahili yanaundwa na maneno pwekepweke ambayo yanaweza kujitegemea kimuundo na kimaana. Aidha, maneno hayo huwa na uhusiano wa kimuundo, ambapo neno moja huwa kuu na huteua neno lingine la kuambatana nalo. Neno dogo ambalo linateuliwa hukumusha neno kuu. Kutokana na uhusiano huo, kunaweza kuwa na uangavu wa maana kutokana na maneno yaliyounda neno hilo (Hassan na Kahigi, 2022). Maneno ambatani sahili hayatenganishwi katika mpaka wa neno moja na lingine (Mfaume, 1985; Hassan na Kahigi, 2022) kwa sababu uambatanishaji hutumia maneno kamili kama malighafi kuunda maneno mengine mapya kabisa (Ayiega na Mwita, 2021).

Kwa upande mwingine, maneno ambatani changamani huundwa kwa mchanganyiko wa mofu huru na mofu tegemezi, ambapo kimojawapo kinaweza kuanza katika neno (Ralli, 2013). Maneno ambatani huandikwa kwa namna tatu: kuunganisha maneno (mawili) pamoja, kuunganisha kwa kutumia vistariungio na kuacha nafasi kati ya maneno yaliyoambatanishwa. Uandishi huu wa maneno ambatani kwa namna tofauti unaukiliwa na aina ya uambatanishaji, ikiwa ni sahili au changamani. Katika makala haya, kwa kuwa kinachojadiliwa ni makosa ya kutenganisha maneno, maneno ambatani yanayotakiwa kuandikwa bila kuachwa nafasi ambayo ni yale sahili ndiyo yaliyojumuishwa. Namna zingine za uwasilishaji wa maneno ambatani hazijajadiliwa kwa sababu sio lengo la makala haya. Makala yanaonesha kuwa waandishi hutenganisha neno ambatani sahili bila kuzingatia kwamba, baada ya kuundwa, linakuwa neno moja linaloandikwa bila kuachwa nafasi na sio maneno kadhaa. Jedwali Na. 4 linaonesha maneno ambatani yanavyotenganishwa na waandishi:

**Jedwali Na. 4: Utenganishaji wa Maneno Ambatani**

| Na. | Neno Lililotenganishwa | Matini Lilimotokea |
|---|---|---|
| 1. | miundo mbinu (miundombinu) | Ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni unakwamishwa na **miundo mbinu** isiyo rafiki. |
| 2. | umbo asili (umboasili) | Umbo asili la neno kioo ni kilolo. |
| 3. | umbo sauti (umbosauti) | Fonolojia (umbo sauti) inahusu vitamkwa ambavyo ni konsonanti na irabu. |
| 4. | isimu jamii (isimujamii) | Uitaji wa majina ni kitengo kimoja wapo katika isimu jamii. |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2023)

Jedwali Na. 4 linaonesha maneno ambatani yametenganishwa badala ya kuandikwa bila kuacha nafasi. Makala yanaonesha kuwa huu ni ukiukaji wa uandishi sahihi na sanifu wa maneno hayo. Kwa hiyo, uandishi huu, pamoja na kwamba hauharibu maana ya maneno hayo, unasababisha uholela katika uandishi wa maneno hayo na kukiuka utaratibu wa lugha ya Kiswahili wa kuunganisha maneno ambatani sahili. Kwa hiyo, maneno haya yanaweza kusomeka kwa namna tofauti na kusababisha wasomaji wakose msimamo kuhusu uandishi sahihi wa maneno ya namna hii. Lugha yoyote ile inaongozwa na kaida zake. Kwa hiyo, ni vema kaida za lugha zizingatiwe ili kuondoa tofauti na mvurugano katika matumizi. Ingawa kuna maneno ambatani ambayo huandikwa kwa kuachiwa nafasi, ni vema kanuni ya kutotenganisha maneno ambatani sahili pia ikazingatiwa (Mfaume, 1985; Hassan na Kahigi, 2022).

## 4.2 Kuunganisha Maneno

Kosa la kuunganisha maneno linahusu maneno mawili au zaidi kuandikwa pamoja bila nafasi yoyote kuachwa baina yake (Kohsom na Gobet, 1997; Stephano, 2019). Utenganishaji wa maneno hurahisisha utambuzi wa haraka wa maneno na kuongeza kasi katika usomaji (Oralova na Kuperman, 2021). Matokeo yanayowasilishwa katika makala haya yanaonesha maneno yaliyounganishwa kimakosa ni ya aina mbili. Aina ya kwanza ni maneno yanayotanguliwa na kitenzi shirikishi cha "kuwa na" na aina ya pili ni viunganishi tegemezi vinavyoanza na "kwa".

### 4.2.1 Maneno Yanayotanguliwa na Kitenzi Shirikishi "kuwa na"

Vitenzi shirikishi huonesha uhusiano baina ya vitu (nomino), na hali, tabia au mazingira fulani (Mohamed, 1998; Habwe na Karanja, 2004). Vitenzi shirikishi vya "kuwa na" huonesha ushirikisho wa vitu. Huonesha kwamba mtu fulani anamiliki kitu fulani, au kitu fulani kinamiliki kitu fulani (Mohamed, 1998). Kitenzi hiki, kwa hiyo, huwa na mofu "na" mwishoni ambayo ndiyo huashiria umilikiwa wa kitu hicho. Matokeo ya utafiti yanayowasilishwa katika makala haya yanaonesha kuwa waandishi wanaunganisha maneno yenye vitenzi hivi na maneno yanayofuata. Uunganishwaji huu unaoneshwa kwa mifano iliyomo katika Jedwali Na. 5:

**Jedwali Na. 5: Uunganishaji wa Maneno Yanayotanguliwa na Kitenzi Shirikishi cha "kuwa na"**

| Na. | Neno Lililounganishwa | Matini Lilimotokea |
|---|---|---|
| 1. | unalengo (una lengo) | Mkabala huu **unalengo** la kuonesha jinsi lugha ya pili inavyo athiriwa na lugha ya kwanza. |
| 2. | kinalengo (kina lengo) | Kipengele hiki **kinalengo** la kujadili dhima za lugha. |
| 3. | wanahaki (wana haki) | Wanafunzi wanao andika vizuri **wanahaki** ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | kupongezwa. |
| 4. | zinaupungufu (zina upungufu) | Fasili hizi **zinaupungufu** kwasababu zimeegemea upande mmoja. |
| 5. | anauwezo (ana uwezo) | Mjifunzaji wa lugha **anauwezo** wa kutabiri kanuni kwa sababu ya kujumuisha. |
| 6. | inatabia (ina tabia) | Lugha **inatabia** ya kuathiri na kukubali kuathiriwa kutokana na mwingiliano wa lugha. |
| 7. | inahazina (ina hazina) | Ni dhahiri kuwa Afrika **inahazina** kubwa ya utamaduni uliokitwa katika majina. |
| 8. | inamaana (ina maana) | Hii **inamaana** kwamba jamiilugha hutofautiana kwa kila kitu. |
| 9. | yanauhusiano (yana uhusiano) | Bila shaka majina hayo **yanauhusiano** na jamii. |
| 10. | inamatumizi (ina matumizi ) | … lugha **inamatumizi** na umuhimu wake katika jamii … |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Data zilizomo katika Jedwali Na. 5 zinaonesha kwamba vitenzi shirikishi vya "kuwa na" vinaunganishwa na maneno yanayofuata, hasa nomino. Data zinaonesha zaidi kuwa waandishi hudhani kwamba "na" iliyopo mwishoni mwa kitenzi ni kiambishi cha njeo ya wakati uliopo hali timilifu. Kiambishi hiki cha njeo, kama ilivyo viambishi vingine, ni kiambishi awali ambacho huungana na viambishi vya ruwaza zingine kukamilisha uambishibainishi wa kitenzi cha Kiswahili. Kwa hiyo, kiambishi cha njeo ya wakati uliopo lazima kitokee katika kitenzi na si katika aina zingine za maneno kama vile nomino, kama inavyofanywa na waandishi. Nafasi ya kiambishi hiki inaweza kukaliwa na viambishi vingine vya njeo kama vile *-li-* (kiambishi cha njeo ya wakati uliopita), na *-ta-* (kiambishi cha njeo ya wakati ujao), pamoja na viambishi vya hali kama vile *-me-* ambacho ni kiambishi cha hali timilifu. Katika makala haya, inafafanuliwa kuwa, kama ambavyo haiwezekani kuweka viambishi vingine vya njeo na vya hali katika mfuatano wa vitenzi shirikishi vya "kuwa na" na nomino (mathalani ***ali****haki*, ***ata****haki*; na ***ili****tabia*, na ***ita****tabia)*, ndivyo ambavyo pia haitakiwi kukichukulia kiambishi "*na*" cha kitenzi shirikishi kama kiambishi cha njeo katika mfuatano wa maneno wa aina hiyo.

### 4.2.2 Viunganishi Tegemezi Vinavyotanguliwa na "kwa"

Viunganishi tegemezi ni vile vyenye vipashio ambavyo havilingani hadhi kimuundo (Kihore, 2009). Kipashio chenye kiunganishi tegemezi hushushwa hadhi na kuwa tegemezi kwa kipashio kisicho na kiunganishi cha aina hiyo (Mgullu, 1999). Viunganishi hivi ni kama vile **ikiwa**, **kama**, **kwa vile**, **ijapokuwa**, **kwa kuwa**, na

**kwa sababu**. Baadhi ya viunganishi tegemezi huandikwa kama maneno mawili. Viunganishi tegemezi huwekwa mwanzoni au katikati mwa sentensi. Nafasi yoyote vinapowekwa, viunganishi hivyo havibadili dhima yake ya kuhusisha vipashio husika (Kihore, 2009). Jedwali Na. 6 linaonesha baadhi ya viunganishi hivyo vinavyoandikwa kwa kuunganishwa:

**Jedwali Na. 6: Kuunganisha Viunganishi Tegemezi Vinavyoandikwa kwa Kuachwa Nafasi**

| Na. | Maneno Yaliyonganishwa | Matini Yalimotokea |
|---|---|---|
| 1. | Kwakuwa (kwa kuwa) | Katika maelezo yake anadai kwamba, **kwakuwa** Kiswahili kimetokana na lugha mbalimbali … |
| 2. | Kwasababu (kwa sababu) | Kuna nadharia kadhaa ambazo pia huitwa nadhariatete **kwasababu** hazijafikia kiwango cha unadharia. |
| 3. | Kwavile (kwa vile) | Kwavile lugha hizi zinaunasaba ndio maana zipo katika kundi moja. |

**Chanzo: Data** za Utafiti (2023)

Data zilizomo katika Jedwali Na. 6 zinaonesha jinsi viunganishi tegemezi vinavyounganishwa ilhali vinatakiwa viandikwe kwa kuachwa nafasi baina ya “kwa” iliyopo mwanzoni na sehemu nyingine ya neno inayofuata. Utafiti uliofanyika unaonesha kuwa, kwa sababu viunganishi tegemezi vilivyo vingi huandikwa kwa neno moja bila kuacha nafasi, waandishi hujumuisha, na kujikuta wakiunganisha hata viunganishi visivyotakiwa kuunganishwa. Jambo hili huharibu utaratibu wa uandishi wa maneno hayo na usanifu wa lugha pia. Kwa hiyo, waandishi wanapaswa kuzingatia uandishi sahihi na sanifu wa maneno hayo ya Kiswahili.

## 5.0 Hitimisho

Kwa hakika ni nadra kuandika kila kitu kwa usahihi. Hata hivyo, kuna makosa yanayokithiri, ambapo kutenganisha na kuunganisha maneno ni miongoni mwayo. Makala haya yameonesha kuwa makosa ya aina hii si ya bahati mbaya wala si changamano kwa sababu yanatabirika na yana mwelekeo mmoja, yaani yanatokea kwa namna ileile. Ujirudiaji wa makosa haya kwa namna yenye mwelekeo mmoja unaashiria kwamba kuna kanuni mahususi zinazokiukwa. Ili kuepuka makosa hayo, ni vema uandishi wa vipashio mbalimbali, hasa viambishi na maneno, pamoja na kanuni za uandishi zikazigatiwa vema kulingana na vipashio vya lugha (viambishi na maneno) vinavyojenga tungo husika.

**Marejeleo**

Ayiega, M., na Mwita, L. (2021) “Nomino Ambatani za Kiswahili Zinazokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano”. *East African Journal of Swahili Studies*, Juz. 4(1): 30 - 42.

Booij, G. (2007) *The Grammar of Words: An Introduction to Linguistic Morphology, Second Edition.* New York: Oxford University Press.

Corder, S. P. (1967) “The Significance of Learner's Errors”. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching*, Juz. 5(4):161 -170.

Gass, S. M. & Selinker, L. (2008) *Second Language Acquisition: An Introductory Course*, *Toleo la Tatu*. New York: Routledge Taylor & Francis Group.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Hassan, F., na Kahigi, K. (2022) “Uangavu wa Kisemantiki kama Nyenzo ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Msamiati wa Kiswahili kwa Wageni: Mifano Nomino Ambatani na Nyambuzi”. Katika P. Mtesigwa, na E. Duwe (Wah.), *Kiswahili katika Anga za Kimataifa*. Dar es Salaam: TATAKI na BAKITA. kur. 91 - 124.

Khamis, A. (2009) *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi 1.* Dar es Salaam: TUKI.

Kiango, J. (1995) “Uundaji wa Msamiati Mpya katika Kiswahili: Zoezi lenye Njia Mbalimbali”. *Kioo cha Lugha*, Juz. 1(1): 46 - 54.

Kiango, J. (2000) *Bantu Lexicography: A Critical Survey of the Principles and Process of Constructing Dictionary Intries.* Tokyo: Institute for the Study of Language and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

Kihore, Y. (2009) *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi 2.* Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y., Massamba, D., na Msanjila, Y. (2012) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, Chapa ya Sita.* Dar es Salaam: TUKI.

Kohsom, C. na Gobet, F. (1997) “Adding Spaces to Thai and English: Effects on Reading”. Proceedings of the 19th Annual Meeting of the Cognitive Science Society: ESRC Centre for Research in Development Instruction and Training.

Lieber, R. (2009) *Introducing Morphology.* Cambridge: Cambridge University Press.

Lupogo, I. (2020) “Kukithiri kwa Makosa Yaliyozoeleka katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu: Uchunguzi wa Makosa Maalumu”. *Jarida la CHALUFAKITA*, Juz. 2: 1 - 17.

Mfaume, G. (1985) *Misingi ya Isimu ya Lugha ya Kiswahili*, *Chapa ya Tatu.* Dar es Salaam: Utamaduni Publishers.

Mgullu, R. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Mnenuka, A. (2010) Dhima ya Uradidi katika Mawasiliano ya Kiswahili: Uimarishaji na Udhoofishaji wa Maana. *Kiswahili*, Juz. 73: 32 - 44.

Mohamed, A. (1998). *Sarufi Mpya.* Dar es Salaam: Press and Publicity Center.

Mpemba, T. (2018) “Matatizo ya Uandishi katika Kiswahili: Maana, Chanzo na Ufumbuzi”. Katika S. Omari, na M. Samwel (Wah.), *Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika*. Dar es Salaam: TATAKI. kur. 442 - 474.

Mushumbwa, A. (2022) “Makosa ya Lugha katika Vyombo vya Habari Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Televisheni”. *Nuru ya Kiswahili*, Juz. 1(2): 135 - 163.

Oralova, G. na Kuperman, V. (2021) “Effects of Spacing on Sentence Reading in Chinese”. *Frontiers in Psychology*, Juz. 12: 1- 12. Inapatikana katika https://doi.org/10.3389/fpsyg.2021.765335. Ilisomwa tarehe 6 Novemba 2023.

Polomé, E. (1967) *Kiswahili Language Handbook.* Washington D.C: Center for Applied Linguistics.

Ralli, A. (2013) *Compounding in Modern Greek.* Rio-Patras: Springer.

Rubanza, Y. (1996) *Mofolojia ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Stephano, R. (2019) “Kasoro katika Machapisho: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya *Aya za Shetani*”. Katika A.S. Ponera na Z.A. Badru, *Koja la Taaluma za Insia*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited. kur. 557 - 586.

TET. (2019) *Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita: Lugha na Sarufi.* Dar es Salaam: TET.

TUKI. (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la Nne*. Nairobi: Oxford University Press.

Wangila, L. (2017) *Athari za Arafa kwa Stadi ya Kuandika katika Shule za Kaunti Ndogo ya Bungoma Kusini*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma.